

5. أَلِفَاتُ حَيِّ طَهْرٍ - Alifaatu-Hayyin-Twahur

Ni مَدُّ الطَّبِيعِي (maddutw-twabiy'iy) inayotokana katika kutamkwa baadhi ya الحُرُوفُ الْمُتَقَاتَةُ (Al-Huruwf Al-Mutaqatw-twa'ah)¹ zinazoanzia baadhi ya Suwrah, kwa vile herufi hizo zinatamkwa kama herufi za hijaiyah حَا يَا طَا هَا رَا . Nazo zimeundwa katika ibara ya حَيِّ طَهْرٍ (hayyun twahur) kwa jina jingine huitwa أَلِفَاتُ حَيِّ طَهْرٍ (Alifaatu hayyin twahur).

Mfano:

Suwrah	Huruwf Al-Mutaqatw-twa'ah	Herufi
Suwrah saba zinazoanzia	حَم	ح
Maryam Yaasiyn	كَهَيْعَصَ يَسَ	ي
Twaaha, An-Naml, Ashu'araa, Al-Qaswasw	طَه طَسَ طَسَمَ	ط
Maryam, Twaaha	كَهَيْعَصَ طَه	ه
Yuwnus, Huwd, Yuwsuf, Ar-Ra'd, Ibraahiym, Al-Hijr	الر	ر

¹ Rejea mlango wa Maddul-Far-'iy - Al-Madd Al-Laazim Al-Harfiyy